# UNIVERSITY JOURNAL

*ISSN: 2507-7864*



## EDITORIAL BOARD

| | |
|---|---|
| Prof.Yunis Abdille MUSA | Chief Editorial Board |
| Prof. Fowzi Mohamed Barrow | Editor |
| Prof.Msafiri Mshewa | |
| Prof.Mohamed Ali El-Kamil | |
| Mr.Burhan Hatinbu muhuzi | |
| Mr. Mohamed Haji Ali | |
| Mrs.Mwanatumu Ali Hassan | |

Advisor Board

| | |
|---|---|
| Prof. Amran Mohamed Rasli | (Chairman) SUMAIT University |
| Prof. Hamed Rashid Hikmany | SUMAIT University |
| Prof. Mustafa Adam Rushash | Zanzibar University |
| Prof. Said Ahmed Moh'd. | The State University of Zanzibar |
| Prof. Mohammed Al sheikh | The State University of Zanzibar |
| Dr. Miraji Ukuti Ussi | Commission for tourism, Zanzibar |
| Dr.Nassor Hamad Bakari | SUMAIT University |
| Dr. Mohamed Saleh Abdala | SUMAIT University |



**The Chief Editor,**
**SUMAIT University Journal of Scientific Studies,**
**P.O. Box 1933,**
**Zanzibar, Tanzania**
**Ph. +255-24-223-9396**
**E-mail:** sumaitcrpc@gmail.com
**Website: http:/journal.sumait.ac.tz**



**Annual Subscription: USD 5 (2 issues) for institutions,And USD 40 (2 issues) for individuals**

**ISSUE NO:5 DECEMBER 2018**

# MBANO KATIKA HADITHI FUPI: MFANO WA HADITHI FUPI YA *DAMU NYEUSI*

Dkt. Masoud Nassor Moh'd♣

**Abstract**

*Short story is one among the written literature genres which, for a long time has been neglected. However, recently, and as far as Kiswahili literature is concerned, the genre is growing rapidly. Short stories, like any other literary genres, have their peculiar features. One of the key features, which unfortunately many literary critics are not aware about it, is compression. This is the feature that differentiates short stories from other forms of fictions such as novel. This paper, therefore, aims at discussing the importance of compression as a key feature of short stories citing examples from a Ken Walibora's Kiswahili short story* ***Damu Nyeusi*** *in collection* ***Damu Nyeusi na Hadithi Nyengine.***

**Ikisiri**

Hadithi fupi ni utanzu wa fasihi andishi ulioachwa nyuma kwa muda mrefu, katika fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, utanzu huu umeibuka na kukua kwa kasi kubwa katika miaka ya hivi karibuni. Utanzu huu, kama zilivyo tanzu nyengine za fasihi andishi, una misingi na muundo wake. Unajengwa kwa sifa zake bainifu ambazo mara nyingi hazipatikani katika tanzu nyengine. Sifa yake moja kuu ni kipengele cha mbano. Kipengele hiki ndicho kinachoifanya hadithi fupi ionekane fupi lakini yenye ukamilifu wa taarifa na maudhui aliyoikusudia mwandishi. Kwa bahati mbaya, kipengele hiki hakieleweki vya kutosha miongoni mwa wachambuzi wengi wa hadithi fupi za Kiswahili. Makala hii inafafanua kipengele hiki, huku ikitumia hadithi fupi ya *Damu Nyeusi* iliyomo katika mkusanyo wa *Damu Nyeusi na Hadithi Nyengine*. Makala hii ni muhimu kwa kuwa inatarajiwa kutoa mwanga wa kutosha juu ya kukielewa na kukitumia kipengele cha mbano katika uandishi na uchambuzi wa hadithi fupi za Kiswahili.

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ya Kiswahili imepita katika historia ndefu ya uanzaji na ukuaji wake. Kama zilivyo fasihi za jamii nyengine, nayo ina historia yake thabiti na halisi. Kinyume na maoni ya baadhi ya watu, hususan Wazungu kwamba eti Waafrika hawana fasihi au fasihi yao ni finyu mno. Ilivyo sahihi, jamii za Kiafrika wakiwemo Waswahili, wamesheheni tanzu mbalimbali za fasihi simulizi na andishi. Kwa upande wa fasihi andishi, Waswahili wana tanzu kama vile mashairi, riwaya, tamthiliya, hadithi fupi,

♣ Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar( SUZA)

wasifu pamoja na tawasifu. Kila utanzu kati ya tanzu hizi unayo historia yake inayoelezea namna utanzu huo ulivyoanza, ulivyo sasa na unavyoendelea kubadilika siku hadi siku.

Hadithi fupi ni utanzu wa fasihi andishi unaowatatiza waandishi wengi kuutolea maelezo ya fasili yake. Hata hivyo, wapo wataalamu wengi waliojaribu kuzungumzia ugumu wa fasili yake, historia yake na kueleza sifa zake. Miongoni mwa wataalamu waliyoielezea hadithi fupi kwa namna mbalimbali ni kama vile; Austin Wright (1989), Todorov (1975), Friendman (1989), Rohrberger (1982), Charles May (1995), Burges (1984), O'rourke (1989), Ferguson (1982), Pratt (1994), Mathews (1964), bartens (2003) Indangasi (1998), Esenwein (1909), Wales (2001) Stefan Colobaba (2010) na Poe (1938). Kila mmoja miongoni mwa wataalamu hawa, ameeleza mtazamo wake juu ya dhana mbalimbali zinazohusu utanzu wa hadithi fupi, unaochunguza katika makala hii.

Tukichukulia mfano mmojawapo wa mhakiki maarufu wa hadithi fupi Edgar Allan Poe (1938) yeye anasema:

> *Hadithi fupi si sura katika riwaya, tukio wala kituko ambacho kimechopolewa katika hadithi ndefu, au kisa kirefu, bali ni utanzu ambao humvutia na kumteka msomaji, kumfanya aamini kuwa ingeweza kuharibika ikiwa itakuzwa na kuwa ndefu, au kama itafanywa sehemu ya kazi kubwa*. (Tafsiri)

Maelezo ya Poe hapo juu, kuhusu dhana ya hadithi fupi kwa maoni yangu, yana ukweli dhahiri. Hii ni kwa sababu, kweli kuna baadhi ya watu hudhani kuwa, hadithi fupi si utanzu unaoweza kutafautishwa kwa sifa zake bainifu, na kwamba tunaweza kuchukua sehemu ya riwaya tukaifanya hadithi fupi. Jambo hilo haliwezekani hata kidogo. Hadithi fupi, ni utanzu unaowiyana na riwaya kwa aina ya lugha tu yaani unathari, lakini unajitofautisha kwa sifa nyengine kadhaa kama vile mbano, uteuzi wa maneno, umoja, na uharaka wa kulieleza lengo la hadithi hiyo.

Poe (ameshatajwa) anaieleza sifa mojawapo ya hadithi fupi kuwa, ni utanzu uliyo mfupi unaowezekana kusomwa kwa kikao kimoja tu. Aidha kimaudhui, anasisitiza kuwa lengo la hadithi fupi kwa desturi, huwa ni kuzua athari moja kuu iliyo ya kipekee, yaani huwasilisha dhamira moja kuu. Upekee huu unaufanya utanzu huu kujitegemea na kujitofautisha na tanzu nyengine kama vile riwaya.

Naye Esenwein (1909:51) ameandika hivi:

> *Hadithi fupi ni maelezo mafupi, ya kubuni, yanayotokana na tukio moja linaloongozwa na tabia moja ya mhusika mkuu. Ina muundo,*

*na maelezo ambayo yamebanwa na mpangilio uliopangwa vizuri, ili kuibuwa hisia moja kuu. (TY)*

Alichomaanisha Esenwein ni kuwa, hadithi fupi ni hadithi ya masimulizi ya kubuni, inayozungumzia tukio moja kuu, na ina mhusika mkuu mmoja. Huwa na muundo maalumu uliokitwa katika mbano wa hali ya juu ili kuleta hisia moja kuu kwa msomaji.

Utanzu huu wa hadithi fupi, msingi wake unahusishwa kwa kiasi kikubwa na mhakiki wa Kimarekani aitwaye Edgar Allan Poe. Kwa upande mwengine, Brander Mathew (1964) anaaminika ndiye aliyelitumia neno la Kiengereza ‘’short story’’ kwa mara ya kwanza.

Wamitila (2003: 54) anaielezea hadithi fupi kuwa, ni ile ambayo inashughulikia suala fulani kwa muhtasari na huwa aghalabu na mhusika mkuu mmoja anayejitokeza waziwazi ingawa hakuzwi kama ilivyo katika novela au riwaya. Anaendelea kueleza kuwa, hadithi fupi haina upana wa kimaudhui wala uchangamano wa kimuundo, kama ilivyo katika tanzu nyingine za kinathari.

Naye Mohochi (1997) anafafanua kuwa, utanzu wa hadithi fupi umepuuzwa ingawa ni muhimu sana katika jamii ya sasa, kama zilivyo muhimu tanzu nyengine za fasihi andishi. Kwa ujumla, kwa maoni yangu tunaweza kusema kuwa, hadithi fupi ni utanzu mfupi wa kinathari unaojishughulisha na suala fulani kuu au wazo kuu moja. Huwa na wahusika ambao hawakuzwi kwa kina na unaotumia mbinu ya kimaelezo ya kibanifu zenye uelekezi wa kiwango cha juu, hautanui mandhari yake na unasifika kwa sifa ya umoja.

## 2.0 Mbinu za Uchambuzi wa Hadithi Fupi.

Uchambuzi wa matini ya kifasihi ni kazi anayojipa mtu mwenyewe, kwa lengo la kutazama na kuchuja kazi ya fasihi, na kuionesha kazi hiyo namna ilivyoundwa katika vipengele vyake mbalimbali. Kila mchambuzi wa kazi ya fasihi ni lazima azingatie aina ya utanzu anaouchambua. Hii ni kwa sababu kila utanzu una namna na taratibu zake za kiuchambuzi zilizotafauti na utanzu mwengine. Kwa sababu hiyo, kuna uwezekano wa kukosa ufanisi wa kiuchambuzi iwapo mchambuzi hatatumia maarifa ya uchambuzi ya utanzu anaoushughulikia.

Kwa kawaida matini ya kifasihi ipo katika pande mbili; fani na maudhui. Kwa hivyo, mchambuzi inampasa tangu mwanzo ajiulize, ni upande gani anaolenga katika kuufanyia uchambuzi wa kifasihi kwenye matini yenyewe? ni fani au maudhui? Ingawa hivyo, kazi za wachambuzi wengi zimejikita katika kushughulikia upande wa maudhui kiasi cha kusahau kwamba upande wa fani ni muhimu vilevile uchambuliwe. Matokeo yake, vipengele kadhaa vya kisanaa vimebezwa na

kudharauliwa kabisa katika fasihi ya Kiswahili. Miongoni mwa vipengele hivyo katika utanzu wa hadithi fupi ni mbano. Hivyo, makala hii imezingatia kwa undani namna mbano unavyojitokeza katika utanzu wa hadithi fupi.

### 3.0 Dhana ya Mbano katika Hadithi Fupi.

Kulingana na Mohamed (1995), mbano ni mshikamano na mpatano wa elementi zinazoijenga kazi ya fasihi. Mbano unapojengwa vizuri unasaidia muwala na muumano wa kazi ya fasihi Unaifanya kazi hiyo ionekane vizuri katika upatanifu wa vipengele vyake mbalimbali; neno na neno, sentensi na sentensi, wazo na wazo na kipengele kimoja na kingine. Kazi ya kifasihi iliyokosa mbano hupoteza upatanifu na muumano wa elementi zilizoijenga kazi hiyo. Matokeo yake, unaweza kuona baadhi ya vipengele visivyo na mchango wowote katika ujenzi wa kazi hiyo. Kwa mfano kazi hiyo inaweza kuwa na wahusika wasio na kazi maalumu pamoja na matumizi ya msamiati ambao hauna mchango uliyowazi katika hadithi hiyo.

Naye wamitila (2002), anaeleza kuwa, hadithi fupi huwa na urefu mahususi ambao unazuwia kuwepo kwa sifa zinazopatikana katika tanzu nyengine za fasihi kama vile riwaya. Hadithi fupi hubanwa sana, kiasi kwamba, mwandishi hatakiwi kutoka nje ya mada anayoizungumzia. Mwandishi wa hadithi fupi analazimika kuwakuza wahusika wake waonekane kama wahusika waliokuzwa kikamilifu kwa njia ya haraka sana. Ingawa huwa tunawaona kwa kipindi kifupi, tunahisi kuwa wamekamilika kabisa. Mtunzi wa hadithi fupi analazimika kujifunga kwenye mada kuu, bila ya kuyashughulikia masuala ambayo hayana mchango kwenye mada kuu ya hadithi yake. Halikadhalika, hadithi fupi haitarajiwi kutumia mbinu rejeshi kwa upana kama ilivyo katika utanzu wa riwaya au tamthilia ambapo urejeshi hutawala au hutumika kwa wingi.

Utokaji nje ya hadithi huisaidia sana riwaya katika kutamba na kutambaa kwake, katika hadithi fupi, jambo hilo huwa halina matokeo mazuri hata kidogo. Kwa hivyo, mbano ni sifa na kipengele muhimu sana katika utunzi na uchambuzi wa hadithi fupi. Mbano unajengwa na vipengele kama vile; wahusika, uteuzi wa majina ya wahusika, mandhari, uteuzi wa msamiati na lugha kwa jumla. Makala hii imetumia hadithi fupi ya ***Damu Nyeusi*** iliyomo katika mkusanyo wa ***Damu Nyeusi na Hadithi Nyengine*** kujadili mambo hayo

### 4.0 Muhtasari wa Hadithi ya Damu Nyeusi

Damu Nyeusi ni hadithi iliyoandikwa  na mwandishi mashuhuri wa Kenya; Profesa Ken Walibora na kuchapishwa kwa mara ya kwanza mwaka (2007). Inazungumzia dhamira ya ubaguzi wa rangi katika nchi za Wazungu hususan Marekani. Ni katika nchi hiyo, ambapo mandhari ya hadithi hii yametumika. Hadithi inasawiri dhana ya

ubaguzi wa rangi kwa kiasi kikubwa. Inaonesha namna watu weupe (Wazungu) wanavyowabagua watu weusi (Waafrika) katika kila eneo. Kwa kisingizio hicho cha rangi, Waafrika wanadhalilishwa na kupuuzwa kila mahali. Hawapewi hata fursa ya kusafiri katika mabasi pamoja na Wazungu ingawa wanalipa nauli sawa. Kukithiri kwa hali hiyo, ndiko kulikomsukuma Ken Walibora kuandika hadithi hii na kuiita Damu Nyeusi.

Iwapo tungeichambua hadithi ya Damu Nyeusi maudhui yake, nadharia ya ‘unigrotude’ ingefaa zaidi. Kwa kuwa tunachokiangazia ni kipengele cha kifani, uchambuzi wa mbano katika hadithi hii umefanywa kwa kutumia nadharia ya umuundo, nadharia ya ujumi na pia nadharia ya elimu- mitindo, katika kuchunguza namna mbano ulivyosawirika kwenye hadithi fupi.

**5.0 Vipengele vya Mbano Vilivyochunguzwa na Ufafanuzi wa Kinadharia**.

Katika makala hii vipengele vilivyoteuliwa na kuchunguzwa jinsi vilivyotumiwa na mwandishi kuibana hadithi yake ni; uteuzi wa maneno, Wahusika, mandhari, lugha, matumizi ya usambamba, matumizi ya methali na mbinu ya maswali. Kama ilivyobainishwa awali katika 4.0 uchambuzi wa mbano katika vipengele hivyo, umeongozwa na nadharia ya umuundo iliyoasisiwa na Ferdinand de Saussure. Nadharia hii, inabainisha mjengeko wa umbo la lugha kutokana na miundo mbalimbali ya viwango vilivyo katika daraja za chini. Nadharia ya ujumi ambayo, inazingatia ufundi wa mwandishi katika kusawiri muonekano wa uzuri kwa kila elementi ya hadithi hii nayo pia imezingatiwa. Palipotokezea haja, nadharia ya elimu mitindo inayompa nafasi mwandishi kucheza na lugha apendavyo kulingano na mtindo wa muktadha anaouandikia ilitumiwa vilevile.

**5.1 Uteuzi wa Maneno.**

Uteuzi wa msamiati katika hadithi fupi ni jambo la msingi sana. Uteuzi wa msamiati humsaidia mwandishi kuibana hadithi yake na kuyawasilisha vizuri kwa utoshelevu yale anayoyakusudia. Maneno yakiteuliwa kwa ufundi, huifanya hadithi iwe fupi lakini yenye uzito wa maudhui. Kwa maneno mengine inaweza kusemwa kuwa, hadithi fupi inatarajiwa kuwa na maneno machache lakini yenye maana pana inayowasilisha vizuri dhamira ya mtunzi.

Uteuzi mzuri wa maneno ndio unaifanya hadithi hiyo ibanike. Uteuzi wa maneno usipokuwa mwafaka unaifanya kazi hiyo ipoteze sifa ya mbano, na hivyo, kuifanya kuwa ndefu, urefu ambao hauna tija yoyote. Aidha, kwa upande mwengine, mbano unamlazimisha mwandishi ateue msamiati kwa uangalifu ili kuufanikisha mbano wa hadithi yake. Kwa hivyo, sifa hizi zote zinategemeana na kuumana vizuri katika ujenzi wa matini ya hadithi fupi. Mwandishi wa hadithi hii iitwayo Damu Nyeusi

ameonesha uwezo mkubwa wa kuteua na kuyatumia maneno mahali pake, kila neno aliloliteua na kulitumia limeonekana kuwa ndiyo sehemu yake na limeweza kufanikisha vizuri taswira ya ubaguzi aliyoikusudia.

Kwa mfano mwandishi anasema**;**

> *...kujikomboa kwenye mikatale ya kubaguliwa, kubeuliwa na kudhulumiwa na mtu mweupe...(*Damu Nyeusi:22*)*

Maneno aliyoyatumia katika nukuu hiyo; *kubaguliwa, kubeuliwa na kudhulimiwa* yanaonesha kina cha dharau na ubaguzi uliopo miongoni mwa Wazungu dhidi ya Waafrika. Ubaguzi uliopo sio wa matendo tu bali hata wa maneno na ishara za viungo vya mwili. Neno **kubeua** linaashiria dharau inayoambatana na picha fulani usoni juu ya jambo ulilolishusha thamani. Aidha, katika hadithi hii mwandishi amefanikiwa vizuri kuteua maneno kulingana na maudhui ya hadithi yake. Neno **weupe** ambalo amelitumia mara nyingi katika hadithi hii, limeakisi ule ubaguzi wa rangi unaofanywa na wale wajiitao 'weupe' dhidi ya wale wanaowaita 'weusi'. Kwa mfano mwadishi anasema;

> *Theluji ilikuwa imefunika na kujenga mandhari **nyeupe pepepe** si madirisha, si milango, si paa, si kuta, si majani ya miti, si matawi na mashina, si kando na katikati ya barabara ya magari, si pembezoni na katikati ya vijia vya wapita njia na waendeshaji baskeli- kote **weupe** wa theluji umehanikiza na kufunika kila kitu kama blanketi la unga liliufunika mji. Theluji na barafu kila mahali, kila pahali barafu na theluji, kila kitu **cheupe** katika nchi hii, mtu **mweusi** apate wapi sauti na satua.* (Damu Nyeusi:22)

Pia amesema:

> *...likija basi lingine na ambalo usukani wake umeshikwa na dereva **mweupe** mwenye moyo **mweusi** yumkini mambo yatakuwa yale yale. (Damu Nyeusi:22)*

Ukichunguza katika nukuu hizo, utagundua maneno ya rangi hasa weupe na weusi yametamalaki, maneno hayo mara nyingi, kila yanapotumiwa katika maandiko mbalimbali, huwa yanaashiria ubaguzi. Jamii isiyoendekeza ubaguzi huwezi kusikia maneno hayo yakitajwa mara kwa mara namna hiyo

Katika sehemu nyengine mwandishi anasema;

> *Licha ya kujaribu kulisimamisha, dereva mzungu amejikurupusha kana kwamba hamna kituo rasmi pale cha abiria*... (Damu Nyeusi:22)

Neno *mzungu* katika nukuu hiyo limetosheleza kuwakilisha dhana ya ubaguzi wa rangi uliopo hapo, kutumia neno hilo pasi na kuzungumzia kama pana ubaguzi kumetosha kufasirika hivyo kwa ufasaha zaidi. Vilevile nukuu hiyo, kwa ujumla wake, inaonesha uwezo wa ubanaji wa dhana pana kwa maneno machache.

Aidha katika sehemu nyengine mwandishi anasema;

> *...likija basi lingine na ambalo usukani wake umeshikwa na dereva mweupe mwenye moyo mweusi yumkini mambo yatakuwa yale yale.* (Damu nyeusi:22)

Sentensi hii pia imesaidia kuibana matini ya hadithi hii kwa namna yake kwani imesheheni taswira za kibaguzi ndani yake. Aina hizo za sentensi kwa ufundi mkubwa zimeyafupisha maelezo marefu ambayo pengine yangehitajika katika utanzu mwengine wa fasihi usiyokuwa huu wa hadithi fupi.

Hivyo, kupitia nukuu za hapo juu, tunauona mbano jinsi ulivyowakilishwa kwenye maneno teule yaliyokozeshwa, ambayo kimsingi yana maana iliyo pana. Lau maneno hayo yasingetumika ingempasa, mwandishi aandike msururu wa maneno katika kulielezea kila moja wapo ya maneno hayo teule. Si hasha msururu huo wa maneno ambao ungetumika, ungepoteza sifa ya ujumi na mvuto wa hadithi yenyewe. Kwa kuwa miongoni mwa mihimili ya msingi ya kazi za kifasihi ni uteuzi wa maneno. Mhimili huo unapokosekana, husababisha kazi inayohusika kuwa hafifu na chapwa.

## 5.2 Mbano wa Wahusika.

Hadithi fupi huwa na wahusika wachache kadiri iwezekanavyo. Mwandishi hapaswi kuweka wahusika wasio na kazi maalumu katika hadithi yake. Wahusika wanaotarajiwa ni wale tu waliobebeshwa dhamira fulani kuu. Wahusika hawa wanaweza kuwa wawili, watatu, au wanne au zaidi kidogo kutegemea na uhalisia wa dhamira ya mwandishi. Kwa mfano katika hadithi ya **Damu Nyeusi** wahusika wake ni Fikirini, Bob, Fiona na Dereva mzungu, ambao wametosha kuwasilisha dhamira ya ubaguzi wa rangi nchini Marekani. Kila mmoja kati ya wahusika hawa amechangia pakubwa katika ujenzi wa dhamira ileile moja ya ubaguzi wa rangi.

Fikirini, mwafrika mweusi yeye ni mwanafunzi katika Chuo Kikuu nchini Marekani. Anabaguliwa na kila mtu kwa sababu ya rangi yake. Bob na Fiona wanaonekana

weusi kwa rangi zao lakini ni weusi vilevile kwa roho zao. Wanawakilisha tabaka la Wamerekani weusi au Waafrika waliyoathiriwa na uzungu. Nao kuwadharau Waafrika wageni wanaotoka Afrika. Dereva Mzungu, huyu ni mtu mweupe anayefanya ubaguzi wa wazi kwa weusi. Anamuacha katika kituo cha basi, abiria anayelipa nauli kwa sababu ya rangi yake. Tazama mfano ufuatao:

> *Basi limemwacha, basi la abiria ambalo linajuzu kusimama kwenye kila kituo rasmi kama hiki. Limemwacha (Fikirini) kwenye baridi ya mzizimo.....''* (Damu Nyeusi:22)

Fikirini anaachwa na basi linaloendeshwa na Mzungu mweupe kwa kuwa yeye ni Mwafrika mweusi. Ni mfano mbaya sana wa ubaguzi unaoendeshwa na weupe. Kwa hivyo, majina machache ya wahusika walioteuliwa kwa umakini, yamesadifu haraka na kwa mbinu yenye nguvu kuuonesha huo ubaguzi wenyewe katika hali mbalimbali. Aidha namna majina ya wahusika hao yanavyofikirisha msomaji katika hadithi hii na yanavyojenga ujumi na mvuto, imesaidia pia kuujenga mbano wa hadithi hii.

Kwa upande mwengine, uteuzi wa majina ya wahusika na hususan jina la mhusika mkuu Fikirini limeleta mvuto wa ajabu sana katika hadithi hii. Jina hili linaleta fikra pana ya kuyafikiria wanayoyatenda wanadamu ulimwenguni. Linamtaka kila mmoja afikirie namna binadamu walivyojivisha uungu na uwezo wa uumbaji. Kujiona wao ni bora na wengine ni watu wasio na thamani yoyote ile, na kwamba hawapaswi kuwa sehemu ya jamii yao. Watu hao kama watachukua muda kufikiri watagundua kuwa wanachokifanya ni upuuzi usiostahiki kufanywa na wao wanaojiita wameendelea.

Jina Fikirini limefumbata mawazo mapana ambayo yangefaa yaelezwe kwa sentensi nyingi kama mwandishi asingemudu kuteua jina hili. Kwa kuwa mwandishi huyu ni bingwa amesadifu vyema kuyabana mawazo hayo ndani ya jina hili moja. Huu ni mbano. Mbano wa hali ya juu uliofumwa na mwandishi wa Damu Nyeusi. Hadithi imebanika vizuri.

### 5.3 Mbano katika Mandhari.

Mandhari ni kipengele chengine kinachobanwa katika hadithi fupi. Mandhari ya hadithi fupi hayatarajiwi kuwa mapana na yaliyochukua muda mrefu. Sehemu ndogo ya kijiografia na muda mdogo wa kiwakati unaweza kutosha kuwasilisha dhamira ya mwandishi. Kwa mfano, hadithi hii (Damu Nyeusi) kiutendaji imehusika na mandhari ya mchana mmoja tu, kuanzia asubuhi wakati Fikirini anasubiri basi katika kituo cha mabasi. Alipolikosa akaamua kutembea kwa miguu masafa mafupi, ndipo alipokutana na Fiona, dada mweusi aliyemchukua nyumbani kwake kwenda

kumfanyia udhalilishaji. Aliporuhusiwa kutoka hapo nyumbani kwa Fiona, hadithi ikawa imemalizika.

Hata hivyo, mwandishi alikusudia kuyahusisha pia mandhari ya Afrika Mashariki kwa namna ya kipekee. Kwa ustadi wa hali ya juu, aliweza kuyabana mandhari hayo kwa kutaja tu baadhi ya vitu vinavyoiwakilisha Afrika Mashariki. Kwa mfano; mwandishi anasema:

> *Alikumbuka siku zake za fahari alipofuatia warangi kwenye kitongoji cha Kibuye jijini Kampala, gongo kwenye vichochoro vya Ubungo, Dar es Salaam na chang'aa kwenye fondogoo la Mathare, Nairobi''* (Damu Nyeusi:22)

Hapo ametaja maeneo matatu ya miji mikuu ya nchi tatu za Afrika Mashariki kwa lengo la kuiwakilisha Afrika Mashariki na watu wake waliyoweusi kwa asilimia kubwa. Pia katika sehemu nyengine anasema;

> *Kila alapo humfanya atamani chakula cha kwao, ugali na mlenda, wali na pilau, matoke na muhogo*...(Damu Nyeusi:22)

Hapo ametaja vyakula mashuhuri vya nchi tatu za Afrika Mashariki. Lengo ni lilelile la kuibana Afrika Mashariki yote kimandhari kwa maneno machache sana. Halikadhalika, katika sehemu nyengine anasema;

> *Alikumbuka dada zake kutoka kanda ya ziwa miongoni mwa Wahaya aliokutana nao alipokuwa anasomea ualimu katika Chuo cha Walimu cha Mwanza. Alikumbuka dada zake Wanyankole alipowahi kuzuru Uganda-Magharibi. Alikumbuka dada zake Wakamba alipokutana nao alipokwenda ziara Kitui.* (Damu Nyeusi:24)

Ifahamike kuwa taifa la Marekani pamoja na mataifa ya Afrika Mashariki yanayo maeneo mengi yenye kuunda miji na vijiji vyake. Katika Damu Nyeusi mwandsihi ameteua na kuyatumia maeneo machache mno ili kudhihirisha uhalisia wa mbano katika kipengele cha mandhari unavyotakiwa uwe kwenye hadithi fupi. Uchache huo wa maeneo ndio unaomfikirisha msomaji kujiuliza maswali haya na yale yahusuyo eneo kubwa lisilotajwa dhidi ya maangamizi yatendwayo. Endapo mwandishi angeteua maeneo mengi na kuyazungumza, hapana shaka yeyote kuwa Damu Nyeusi ingerefuka mno na kupoteza sifa ya mbano inayotakiwa iwemo kwenye kazi za namna hiyo. Hapo ujumi na mvuto wake usingejitokeza katu.

**5.4 Mbano wa Lugha**

Matumizi ya lugha katika hadithi fupi yanahitaji weledi wa hali ya juu, ili kuweza kuibana hadithi katika kipimo kinachohitajika. Uteuzi wa maneno (tumeshauzungumza kwa namna ya pekee kabla), miundo ya sentensi, matumizi ya tamathali za semi, usambamba na mbinu ya maswali ni nyenzo muhimu sana za ubanifu wa hadithi fupi. Katika hadithi ya Damu Nyeusi mwandishi ameonesha umahiri mkubwa wa kuibana lugha kwa kutumia vipengele hivyo, na kuwakilisha mambo mazito na mapana kwa kutumia lugha iliyobanwa.

**5.4.1 Matumizi ya Usambamba**

Kwa mtazamo wa jumla, usambamba ni kipengele cha kifasihi ambacho kinahusisha uwili wa maneno au kirai ili kuwezesha upatikanaji wa muala baina ya mawazo katika sentensi. Usambamba pia unaweza kuhusisha kukaririwa kwa maneno ya msingi na uwiano wa idadi ya silabi katika pande mbili za sentensi. Mbinu hii husaidia sana kupatikana kwa sauti za kimuziki katika uandishi na usomaji.

Naye Frazier (1989) ameueleza usambamba kuwa ni matumizi ya viungo vya lugha katika sentensi ambazo kisarufi huwa sawasawa au zenye kulingana katika muundo wake, sauti zake, maana au mizani zake. Tazama mifano ya usambamba katika semi za Kiswahili zifuatazo:

a) Haba na haba hujaza kibaba
b) Hisani hailipwi kwa nuksani
c) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
d) Usione nasinzia usemayo nasikia
e) Mwema wako ndiye mbaya wako
f) Akumurikaye mchana usiku atakuchoma
g) Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

Ukizichunguza semi hizo, utaziona zimechukua umbo la usambamba. Kwa mfano (*asiyesikia la mkuu*) na (*huvunjika guu*) ni pande mbili za semi zilizo wiana kiusambamba. Vipande hivyo vinawianao kimizani na vina vya mwisho katika kila kipande.

Hali kama hiyo hujitokeza pia katika nathari ya Kiswahili. Ni mbinu nyengine inayotumiwa na waandishi kuyafupisha na kuyabana mawazo yao ili yawe katika muonekano mfupi wenye uzito. Katika kuonesha uwezo wake wa kuitumia lugha kwa njia ya mbano mwandishi wa hadithi ya *Damu Nyeusi* ametumia usambamba ambao ukifafanuliwa unaweza kutoa mtazamo mpana sana juu ya suala la ubaguzi wa rangi. Kwa mbinu ya usambamba mwandishi anasema:

> *Theluji ilikuwa imefunika na kujenga mandhari nyeupe pepepe si madirisha, si milango, si paa, si kuta, si majani ya miti, si matawi na mashina, si kando na katikati ya barabara ya magari, si pembezoni na katikati ya vijia vya wapita njia na waendeshaji baskeli- kote weupe wa theluji umehanikiza na kufunika kila kitu kama blanketi la unga liliufunika mji. Theluji na barafu kila mahali, kila pahali barafu na theluji, kila kitu cheupe katika nchi hii, mtu mweusi apate wapi sauti na satua?* (Damu Nyeusi:22)

Dondoo hili lenye matumizi makubwa ya usambamba limefumbata mawazo mapana ya kibaguzi miongoni mwa wanadamu wa eneo linalozungumiwa. Usambamba umetumika kuonesha kuwa ubaguzi haupo katika maeneo machache tu katika nchi hiyo, bali kila mahali umejaa. Barabarani, njiani, majumbani, maofisini, katika vyombo vya usafiri na sehemu nyengine kila mahali. Pamoja na wingi wa vitendo vya kibaguzi alivyokusudia kuvionesha mwandishi, matumizi ya usambamba yamemuwezesha kutumia maneno machache kiutoshelevu. Hivyo ni wazi kuwa usambamba ni nyenzo muhimu ya mbano katika hadithi fupi.

Mwisho wa maelezo yake amegusia suala la majivuno ya weupe dhidi ya weusi. Rangi ambazo si chochote si lolote kwa wanadamu zaidi ya utambulisho tu.

**5.4.2 Matumizi ya Semi**

Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa, semi ni kauli fupi ya kisanaa yenye kubeba maana, mafunzo au ujumbe Fulani kwa jamii (Mulokozi:2017). Mara nyingi kauli hizi huwa na mpangilio maalumu wa maneno unaodokeza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yatokanayo na uzoefu wa maisha ya jamii inayohusika. Ni kauli fupi yenye fikra na busara fulani. Ni viungo muhimu kwa ubunifu wa kazi za fasihi. Kwa mfano:

a) *Mficha ugonjwa, kifo humuumbua.*
b) *Mcheza kwao hutunzwa*.
c) *Haraka haraka haina baraka*.
d) *Mkono mtupu haurambwi.*
e) *Mkamia maji hayanywi*.

Ken Walibora mwandishi wa hadithi ya Damu Nyeusi katika kuhakikisha anaibana hadithi yake ametumia baadhi ya methali kama vile;

1. *Nyumbani ni nyumbani ingawa pangoni.* (Damu Nyeusi:24)
2. *Baharia wa pemba kufa maji mazoea.* (Damu Nyeusi:26)

Methali hizi na nyengine, zimefanikisha vizuri mbano wa matini katika hadithi hii. Methali hizo, zimempunguzia mwandishi kazi ya kueleza na kufafanua kwa urefu sana yale anayoyakusudia. Kama tujuavyo kuwa, semi ni utanzu wa fasihi simulizi unaobeba falsafa na maudhui pana kwa jamii. Unapotumiwa katika kazi ya fasihi kama alivyofanya Ken Walibora, huwa unasadifu vyema kuifinyanga kazi hiyo katika muelekeo huohuo wa uzito na upana wa maudhui ingawa kwa uchache wa maneno.

### 5.4.3 Mbinu ya Maswali

Katika hadithi ya Damu Nyeusi mwandishi ametumia mbinu ya maswali. Maswali aliyoyauliza, ni yale ambayo mara nyingi Waafrika huulizwa wakiwa huko uzunguni. Kimsingi maswali hayo, huwakilisha dhana finyu waliyonayo Wazungu dhidi ya Waafrika. Wazungu wana dhana kwamba Waafrika hawavai nguo au wanaishi juu ya miti. Dhana hii ni ya kuwakandamiza na kuwadhalilisha Waafrika. Jambo hili linadokezwa na mwandishi wa hadithi hii kupitia kwa wanafunzi wenzake Fikirini. Wanafunzi hao wa kizungu, pamoja na walimu wake pale walipomuuliza:

*Je, kule kwenu watu wanavaa nguo?*

*Ulivaa nguo mara ya kwanza ulipotua kwenye uwanja wa ndege hapa Marekani?*

*Je, mwaishi kwenye miti kama tumbiri*?

Maswali haya na mengine yamejenga kwa kiasi kikubwa mbano wa hadithi hii. Bila ya maswali haya mwandishi angelazimika kutumia muda mkubwa na maelezo mengi kufafanua mtazamo wa Wazungu dhidi ya Waafrika. Hivyo mwandishi ametumia maswali hayo kama mbinu ya mbano na kwa kweli amefanikiwa kwa kiasi kikubwa.

## 6.0 Hitimisho

Kwa ujumla hadithi ya Damu Nyeusi, imetungwa kuakisi hali halisi ya ubaguzi katika nchi za Wazungu kimaudhui. Kimuundo, mwandishi amefanikiwa kuibana vizuri hadithi yake kwa kutumia mbinu mbalimbali za kilugha, kimandhari, kiwahusika na nyenginezo zilizofafanuliwa katika makala hii. Kwa maoni yangu, Ken Walibora, mwandishi wa hadithi iliyochunguzwa katika makala hii, anastahiki sifa kwa uwezo aliyouonesha wa kuitumia vyema lugha ya mbano na mbinu nyengine zilizofanikisha dhana ya mbano.

Ni matarajio ya mwandishi wa makala hii kuwa, kwa kuitumia hadithi ya Damu Nyeusi kuchambua na kuijadili dhana ya mbano, imesaidia kwa kiasi kikubwa kueleweka kwa mbano katika hadithi fupi. Kuanzia hapa, hapana shaka, waandishi

na wasomaji wa hadithi watakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya mbano na namna inavyoweza kufanikisha uchambuzi wa hadithi fupi.

**Marejeleo**

Bartens, H (2003) *Literary Theory*: *The Basics*. London, Routledge.

Canby, H. Seidel (1961) '*Free Fiction' in Current Garcia and W.R. Patrick*. Chicago.

Esenwein, B (1961) *What is a Short Story, in Current Gercia and W R Patrick* (eds) What is the Short Story: Chicago, Scott, Fores Man.

Fabb. N (1997) *Linguistic and Literature*. Oxford. Backwell Publishers.

Mathews, B (1964) *The Philosophy of the Short Story*. New York: Long Man.

Mohachi, E (1995) *Fani katika Hadithi Fupi za Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili. Nairobi. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mohamed, S.A (1995) *Kunga za Nathari ya Kiswahili*. Nairobi. East Africa Educational Publishers

Mulokozi, M,.M (2017) Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili. Dar es Salaam. Moconny Printing Press.

Pratt, M. L (1994) *The Short Story: The Long and the Short of it*, in Charles May (ed) the New Short Story Theories. Athens: Ohio UP

Rohrbeger, (1982) *Short Fiction and the Numinous Realm: Another Attempt at Definition*; in Modern Fiction Studies XXVIII, 6

Todorov, Tzvetan. (1977) The Poetics of Prose, Transl. Richard Howard. Ithaca NY: Cornell UP.

Walibora, K na Mohamed S. A (2007) Damu Nyeusi na Hadithi Nyengine. Nairobi. Moran Publishers Ltd.

Wamitila, KW (2003) Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia. Nairobi. Focus Publication Ltd.

Wamitila. K W (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi. Focus Publications Ltd.

Wright, A (1989) On Defining The Short Story: The Genre Question, in Lahafer and Clarey (eds) Short Story at a Crossroads. Baton Rouge: Louisiana State. UP.